# Utekelezaji Maazimio Kikao Kazi cha Tano Waleta tija Serikali Mtandao

Katika hatua ya kuunganisha na kurahisisha huduma za Serikali kupitia Mfumo wa Orodha ya Huduma za Serikali (GSD), zaidi ya michakato 900 ya utoaji huduma imeandaliwa na kuingizwa katika mfumo huo kufikia mwezi Februari, mwaka 2026. Wakati huo huo taasisi nyingine zimeendelea kukamilisha utekelezaji wa michakato ya kuorodhesha huduma zao.

kilichofanyika jijini Arusha Februari 2025, yakilenga kuharakisha mageuzi ya kidigitali katika sekta ya umma.




Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo wakati wa kufunga kikao hicho, Mhadhiri na Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dkt. Florence Rashid, amesema Serikali imepiga hatua kubwa katika maeneo kadhaa yaliyokubaliwa na wadau, katika eneo la Serikali Mtandao.

Amesema, kuingizwa kwa huduma hizo katika mfumo wa GSD kunatarajiwa kuongeza uwazi, kurahisisha upatikanaji wa taarifa na kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma za umma kwa njia za kidigitali.

“Kwa kuweka michakato hii katika mfumo mmoja, tunajenga msingi wa uwazi na uwajibikaji, huku tukirahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wananchi,” amesema.

Katika kuimarisha ubora wa huduma, Dkt. Florence amesema Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejumuisha katika mpango kazi wake mapitio na maboresho ya Mwongozo wa Uboreshaji wa Michakato ya Kibiashara (Business Process Improvement- BPI).

Amesema mwongozo huo utasaidia kurahisisha na kuoanisha utoaji wa huduma katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi na mashirika ya umma.

“Mwongozo huu utakuwa dira ya pamoja katika kuboresha michakato na kuondoa urasimu usio wa lazima,” amesema.

Kuhusu azimio la kuwajengea uwezo watumishi wa umma katika eneo la usalama wa mtandao, Dkt. Florence amesema Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeendelea kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wataalamu wa TEHAMA katika taasisi za umma.

Kwa mujibu wa takwimu zilizowasilishwa, mwaka 2025 wataalamu 135 wa TEHAMA kutoka taasisi 127 walipatiwa mafunzo ya kiufundi, huku taasisi 378 zikifikiwa na mafunzo ya kudhibiti matishio ya kimtandao.

Aidha, wadau walikubaliana kuwa taasisi za umma zitenge rasilimali kuelimisha juu ya usalama wa mtandao kwa watumishi wanaotumia mifumo ya TEHAMA angalau mara moja kwa mwaka, ili kupunguza hatari ya mashambulizi ya kimtandao.

Kuhusu Mfumo wa Majaribio ya Kujipima Mwenyewe, amesema e-GA imebuni mfumo wa Majaribio ya Kujipima Mwenyewe unaojulikana kama ‘Online Self-Assessment Test (OSAT)’, unaowezesha watumishi kufanya tathmini binafsi ya uelewa wao kuhusu masuala mbalimbali, ikiwemo usalama wa mtandao, na kupata mrejesho papo hapo.

Dkt. Florence amesema majaribio ya awali ya mfumo huo tayari yameanza kwa ushiriki wa taasisi kadhaa, huku maboresho yakitarajiwa kufanyika kabla ya uzinduzi rasmi, hatua inayolenga kuongeza uwajibikaji na uelewa wa watumishi kuhusu matumizi salama ya mifumo ya kidigitali.

Kwa upande wa changamoto ya upatikanaji mdogo wa mifumo ya kidigitali vijijini, amesema Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) inaendelea kupanua miundombinu ya mawasiliano ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa na huduma za
mtandao.



Amesema, kukamilika kwa minara 758 ya mawasiliano kunatarajiwa kuongeza kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa mtandao vijijini, na hivyo kupunguza pengo la kidigitali kati ya mijini na vijijini.

Katika hatua nyingine, wadau wamesisitiza umuhimu wa taasisi za umma kujenga uwezo wa kupokea na kutumia teknolojia zinazoibukia katika utoaji wa huduma.

Akizungumzia utekelezaji wake, Dkt. Florence amesema, e-GA kupitia Kituo chake cha Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao, imeanza kuunganisha teknolojia mpya katika mifumo mbalimbali ya Serikali ili kuongeza ufanisi.

ISO/IEC 27001:2022 CERTIFIED | ISO 9001: 2015 CERTIFIED